# Kilio Cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere

**Yasin S. Musa**

Lecturer, Department of Literature, Language and Linguistics, Faculty of Arts and Social Sciences

Islamic University in Uganda

**Furaha Chai**

Professor in the Department of Literature, Language and Linguistics, Faculty of Arts and Social Sciences,

Pwani University, Kenya.

**James O. Onyango**

Professor, Department of Literary and Communication Studies, School of Humanities and Development Studies

Laikipia University, Kenya

**Ikisiri**

*Hotuba ni usemi unaotolewa kwa hadhira kwa njia ya mazungumzo au maandishi kwa uzingatifu wa jambo mahsusi. Miongoni mwa maraisi wa nchi huwa mna waliojaaliwa vipaji vya kiuneni kiasi cha kuwafanya raia wa nchi zao kuyaamini yale wayasemayo na kuyaingiza katika utendaji wa maisha ya kila siku; mintaarafu ni Mwalimu Nyerere; hotuba zake zimegubika lugha makbuli ya Kiswahili. Mwalimu Nyerere alipendelea Kiswahili kitumike katika siasa za kiafrika badala ya lugha nyingine yeyote ya Ulaya kwa uoni kwamba kuendeleza lugha zao si tu kwamba ni kuukumbatia utumwa lakini kuuza utu wa Mwafrika – Bloommaert, 1990. Hotuba zake daima zimekuwa ni mshawasha kwa wasomaji na wasikilizaji kila uchao; hasa kwa jinsi zilivyo tagaza ufahima hususani katika kila nyanja ya maisha ya mwanadamu. Leo yake Mwalimu Nyerere hatunaye tena. Makala haya yameongozwa kwa nadharia ya Balagha (Rhetoric Theory); na madhumuni yake makuu ni kubainisha mbinu za kifani alizozitumia Mwalimu Nyerere kuendeleza maudhui yake kupitia hotuba zake hata ikawa ni abakie katika vinywa vya watu wengi, wakimlilia hadi hivi leo.*

**Maneno muhimu**: *ushawishi wa hotuba za Mwalimu Nyerere, Kiswahili*

## Utangulizi

Mwalimu aliita lugha na lugha ikamwitika katika ulingo wa uneni kisiasa. Hii ni kwa ufahima ambapo Watanzania daima wamekuwa hawamwiishi utamu kila wanapozikumbukia hotuba zake; hususani kwa mbiu yake ya *"**sahau ukabila na udini**"* ambapo lugha ya Kiswahili ilikuwa ni kibebeo cha mawasiliano katika harakati za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni; na Watanzania wakawa ni wenye umoja na amani. Atakumbukwa milele! Mungu amlipe kwa matendo yake!

## Maandishi kuhusu Hotuba


Van (1993) alichanganua hotuba ya kisiasa iliyotolewa na mbunge wa *House of Commons* - aliyeitwa Fox - ambaye alikuwa mwakilishi wa chama cha wahafidhina. Hotuba hiyo ilikusudia kumtetea mkuu wa shule ya Bradfold aliyeandika makala iliyoelekea kuleta mabishano makubwa juu ya elimu yenye msingi wa tamaduni nyingi. Kwa kuchunguza matamko tendi katika hotuba ya Fox, Van (aliyetajwa) aliweza kutambulisha kiwango cha madai yaliyotolewa na kukisia athari zake kwa hadhira mbalimbali. Van alifichua kwamba, wapinzani wa Fox katika bunge walidhihirisha uwongo na upendeleo kwa maelezo yao. Watu wengi nje ya bunge hawakujua uwongo huo, jambo ambalo lilionyesha umuhimu wa mahusiano kati ya vitendo neni kwa ubaguzi wa hotuba ambamo zinatolewa. Van (aliyetajwa) alibaini kwamba, hotuba ya Fox ilieleza hisia zinazostahili kutiliwa maanani kuhusu mandhari hasa kwa kuzingatia kwamba, *House of Commons* imepambwa na ishara za nguvu za serikali za bunge la Uingereza linalorejelewa kama mama wa demokrasia. Utafiti wake ulitoa mwanya wa kielimu katika utafiti huu hasa pale ilipobainika kwamba yeye alichunguza hotuba lakini hakuchunguza hotuba za marais hususani Mwalimu Nyerere katika kubaini

maudhui mahsusi, mbinu za kiisimu na mpangilio uliomo katika hotuba hizo; jambo ambalo utafiti huu uliufanyia kazi.

Gres (1982), alichunguza lugha ya matangazo hasa yale ya televisheni huko Marekani. Alimulika mbinu za kiisimu zinazojitokeza waziwazi katika matangazo kama vile matumizi ya neno "Saidia" katika vishazi. Alibaini kwamba watangazaji hupendelea matumizi ya lugha yasiyo dhahiri. Kwa hakika utafiti wa Gres ulikuwa ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu uligusia suala la ushawishi na ulichangia kubaini sababu zilizotumika ili kuleta ushawishi kwa wasikilizaji wa hotuba za kisiasa.

Matasi (2014) alishughulikia hotuba za ijumaa ambapo alidhihirisha vitendo neni vinavyojitokeza katika hotuba hizo na athari zake kwa wasikilizaji wa Bugisu Mashariki mwa Uganda. Kilichopelekea kufanya hivyo ni malalamishi kwamba baadhi ya maimamu hutoa matamko yenye athari hasi kwa maamuma. Utafiti wake ulibainisha kwamba matamko ya hotuba yalikuwa na athari hasi kwa asilimia 48 huku athari chanya zikiwa na asilimia 52. Mtafiti huyu alitumia nadharia ya vitendo neni iliyoasisiwa na Austin (1962) na kuendelezwa na Searle (1969). Wakadhalika alitumia mbinu ya kiwingididi katika uchanganuzi wa deta yake. Utafiti wa Matasi (2014) ijapokuwa ulishughulikia hotuba; unatofautiana na wangu kwa vile aliangazia hotuba za ijumaa; ambapo utafiti wangu ulishughulikia hotuba za kisiasa. Hata hivyo utafiti wake uliufaa utafiti wangu kwa sababu alishughulikia athari za matamko kwa wasikilizaji wa hotuba kwa hivyo ulikuwa ni kielelezo kwa utafiti huu ambapo uliangalia jinsi wasikilizaji na wasomaji wa hotuba za Mwalimu Nyerere jinsi wanavyoshawishika kutokana na matumizi ya lugha yaliyomo katika hotuba zake.

**Msingi wa Kidhana**




Hotuba zilizohusishwa katika uchunguzi huu ni zile za Nyufa na Tunatoka wapi, Tuko wapi na Tunakwenda wapi - kama sehemu ya utafiti kuhusu hotuba za Mwalimu Nyerere. Mbinu ya kimakusudi ndiyo iliyotumika katika ukusanyaji wa deta ya hotuba wakati ambapo mbinu ya kimtandao, uchunguzi shiriki na mahojiano kundi zimetumika katika kupata deta ya maoni na hisia.

**Misingi ya Nadharia ya Balagha**

Nadharia ya balagha ya Aristotle (367 BK) ndiyo iliyoongoza utafiti huu. Hii ni nadharia ya uchunguzi wa lugha kwa mkabala wa ushawishi. Ifuatayo ni mihimili yake.

(a) **Yaliyomo katika usemi**: Aristotle anamaanisha kumchunguza mneni au matini yake katika kiwango cha Logosi, Pathosi na Ethosi yake; ambapo

(i) **Kiwango cha Logosi**: Hapa anahimiza mchunguzi azingatie vile ambavyo mzungumzi alivyoibua hoja au maswali yenye kumpa msikilizaji kutafakari badala ya kujibu (mbinu ya kuuliza maswali isiyohitaji majibu).

(ii) **Kiwango cha Ethosi**: Aristotle anatoa ufahima kwamba wapo wazungumzaji wenye sifa na tabia zinazowapelekea kuheshimiwa na kuenziwa kabla na baada ya usemi wao kwa hadhira. Hivyo, ni vyema mchunguzi kuzingatia sifa bainifu zifuatazo: Uwezo wa jambo analolizungumzia msemaji, namna anavyolichukulia suala analolizungumzia na ubinadamu alionao mzungumzaji kwa hadhira yake.

(iii) **Kiwango cha Pathosi**: Arisitotle anahimiza mchunguzi atathmini hisia za wapokeaji usemi kulingana na uzito wa hoja zilizomo katika usemi huo.

(b) **Mtindo**: Hapa Aristotle anamaanisha mchunguzi ajikite katika kuangalia vile ambavyo mbinu za kifani zilivyopelekea hotuba au usemi kuwa na ushawishi mkubwa kwa hadhira.

(c) **Mpangilio wa hotuba au usemi**: Kadhalika Aristotle anahimiza mpangilio wa hotuba uzingatiwe. Mchunguzi azingatie (jinsi ambavyo mzungumzaji alivyoanza hotuba au usemi wake kwa hadhira), mwili wa usemi huo (jinsi mzungumzaji alivyojenga na kuendeleza hoja zake) na kisha achunguze vile alivyohitimisha usemi wake.

Kwayo, Aristotle kwa ujumla anahimiza mchunguzi kuangalia jinsi mneni alivyo anza hotba yake (kwa maana ya jinsi anavyokubalika na mitindo anayoitumia); anavyoendeleza (kwa maana ya kuchunguza mbinu za kifani katika maudhui anayoyaendeleza) kisha kuzibaini sifa zake bainifu – kwa hutuba aliyoiwasilisha kwa hadhira yake; huku ikiangaliwa miishio ya kila nukta za hotuba yake na kwa ujumla wake.

**Fahiwa kuhusu Fani ya Balagha**

Kwa mujibu wa Assakakiy (1983) balagha ni ufasaha wa lugha. Ni taaluma inayochunguza usemi ili kudhihirisha umaanisho uliomo ndani yake; ujumi na mambo mengine, kwa kuzingatia muktadha. Balagha inazingatia pia jinsi maana moja inavyoweza kuelezewa kwa njia tofauti ili kupata makusudio fulani. Assakakiy (aliyetajwa) alibaini kwamba, balagha ndiyo huibua nyenzo zinazosaidia kupata mwelekeo faafu na kupata vionjo vya kazi lengwa na kuzalisha weledi wa kifani. Alieleza kuwa mwana balagha anapaswa kuelewa kwamba lugha ni chombo cha mawasiliano, kwa njia mahsusi ili aweze kuathiri wasikilizaji au wasomaji. Mbinu za kiisimu ambazo daima mneni au mwandishi huzitumia ni pamoja na: tashbiha, istiara, tashhisi, takriri, majazi na kadhalika

**Maudhui na Mbinu za Kifani katika Hotuba za Mwalimu Nyerere**

Hotuba zilizochunguzwa na kuchanganuliwa katika makala haya ni: **"Nyufa"** na **"Tumetoka wapi …".** Deta ya utafiti ilikuwa ni Hotuba ya **"Nyufa"** na **"Tumetoka wapi …" (**kwa maandishi na kwa maoni ya wasailiwa). Mbinu ya kithamano ndiyo iliyohusika katika uchanganuzi wa data; lengo likiwa ni kubainisha sifa za lugha zinazowapelekea Watanzania kushawishika kiasi cha kuwafanya wapende kuzisoma na kuzisikiliza hotuba za Mwalimu Nyerere kila uchao; chambilecho *Kilio cha Mwalimu* kwa Watanzania; fani ya balagha ndiyo iliyoangaziwa kama kibebeo cha fani zingine katika hotuba teule zilizochanganuliwa kupitia makala haya; ambapo Nadharia ya Uchunganuzi wa Lugha kwa mkabala wa ushawishi na kwa mihimili yake ya: logosi, pathosi na ethosi inapambanulika kama ifuatavyo:

**Logosi (Maswali ya Kibalagha)**

*"…. amepitapita Mgiriki mmoja hapa anajitapa… eti Tanzania yote iko mfukoni mwake? ...ana mfuko mpana kiasi gani? ...ni mshenzi!*

**Pathosi (Hisia za Hadhira)**

Balagha aliyoitumia Mwalimu ni hisia za kukereka kuhusu mdiplomasia wa Kigiriki alivyojinasibu kwa umma wa Watanzania akisema: "***Serikali yote ya Tanzania iko mfukoni mwake"*** ambapo kwa mwalimu

Nyerere alikereka kwa kauli hiyo hata ikawa akijiuliza: "…eti *Tanzania yote iko mfukoni mwake? …mfuko mpana kiasi gani?*". Kumanisha kwamba mdiplomasia huyo alitumia maneno ya dharau kwa Watanzania; kwamba Watanzania hawawezi kumfanya lolote zaidi ya yeye kuwatenda apendavyo sawa na kilichomo mfukoni mwake ambavyo aweza kukitumia apendavyo. Ndiposa Mwalimu akijiuliza kwa Watanzania akisema: "… nimshenzi! Udhihirisho wa vile alivyokereka; na kuchukuwa hatua ya kumsweka ndani minaajili ya kumfunza adabu. Tambwe ambazo zilimgharimu kwani hata alipoombewa msamaha kupitia nchi jirani, Mwalimu aliujibu umma akisema: "… ***simuachii …ni mshenzi";*** kumpasa atambue kwamba kiburi si maungwana kwa watu wa nchi yao wasiopenda vurugu wenye amani yao, utulivu na uhuru wao kamilifu. Kwayo, Mwalimu alitanabaisha umma wa Watanzania na pengine ulimwenguni kote kutambua kwamba kwa maongozi yake hayupotayari kuishi navibaraka; na kwamba Watanzania daima wapo tayari kuitetea nchi yao kwa hali na mali pasina kumchelea yoyote kwa hadhi na kwa utaifa wake.

**Ethosi (Sifa za Mneni)**

Hakika mwalimu alikuwa ni ameonyesha ujasiri na uzalendo katika maongozi ya nchi ya Tanzania. (Kwa pale alipo watanabaisha Watanzania kuhusu dharau ya mdiplomasia aliyoionyesha kwa Watanzania yakwamba serikali yote ya Tanzania iko mfukoni mwake). Mwalimu aliwataka Watanznia watambue kwamba wanapaswa kusimama kidete kuhakikisha wau wanamna hiyo wanatokomezwa katika mazingira ya Watanzania. Kwa imani kwamba, kufanya hivyo, Watanzania watadumisha amani, utu na uhuru wa nchi yao

---

**Logosi (Maswali ya Kibalagha)**

"... ***Mtu ye yote anayeonekana anapenda sana kwenda ikulu na hata yupo tayari kununua kura ili kufika ikulu ni wa kumkwepa kama ukoma.*** Kwanza, hizo fedha kapata wapi. Mtanzania wa leo hawezi kununua watu bila kwanza yeye kununuliwa. ***Na kama kanunuliwa atataka kuzilipaje? Kazipata wapi?*** Watanzania wote ni masikini tu. Mtanzania anaomba urais wetu kwa hela? ***Amezipata wapi?"*** (uk 27:3, HT3) "... Pili, kama hajanunuliwa, ***kazipata wapi? Kama kakopa, atazirudishaje? Ikulu pana biashara gani mtu akope mamilioni halafu aende ayalipe kwa biashara ya Ikulu?*** Ikulu mimi nimekaa kwa muda wa miaka ishirini na mitatu. ***Ikulu ni pahala pazito. Kuna biashara gani Ikulu?"*** (uk 27:4, HT3)

**Pathosi (Hisia za Hadhira)**

**(**Manzania anayewahonga wapiga kura ili ashinde urais wa nchi**)** Mwalimu alitaka Watanzania wajiulize kumhusu mgombeaji anayenunua watu ili apate kushinda; kwani kwa maisha ya Watanzania ni muhali kupata mamilioni ya pesa minaajili ya kuwanunua wengine kwa ajili ya kushinda uchaguzi wa urais. Kwa mwegemo mwalimu alisema: ***Mtanzania wa leo hawezi kununua watu bila kwanza yeye kununuliwa***; na kwamba ikiwa kanunuliwa ***atataka kuzilipaje?*** **(**kumaanisha atafanya ufisadi ili aweze kuzilipa fedha alizopewa / alipe ihsani?**)**. Hali ambayo ilimpasa: mwalimu akijiuliza tena na tena: ***Watanzania wote ni masikini tu. Mtanzania anaomba urais wetu kwa hela?*** Mwalimu aliwataka Watanzania watafakuri kuhusu wagombea wa namna hiyo; huku akijiuliza kwa balagha takriri: ***Kazipata wapi?, Amezipata wapi?, Kama kakopa, atazirudishaje?*** (kwa maana ya Watanzania wajiepushe na watu wanaotaka kulaghai na ama vibaraka wanaotumiwa; kwani wanunuliwao kwa uchu wa madaraka haitakuwa simile kwao kuiambakisha nchi kwa maslahi yao binafsi; kwa uoni wa vile pasivyo na namna ya kuweza kujipatia fedha za kiholela minaajili ya utajirisho na kuwatajirisha wengine kwa hila; kwa ithibati akiwatanabahisha Watanzania kwa kusema: ***Ikulu pana biashara gani mtu akope mamilioni halafu aende ayalipe kwa biashara ya Ikulu? Ikulu mimi nimekaa kwa muda wa miaka ishirini na mitatu. Ikulu ni pahala pazito. Kuna biashara gani Ikulu?"*** Kauli ambazo zilikuwa ni wito kwa Watanzania watambue kwamba watu wa namna hiyo huwa wanatumiwa na wahujumu / mabepari kutoka nje ya nchi, wakidhani kutopelea kwa maendeleo yaliopo kwa Watanzania kutakuwa ni njia faafu ya kuyapitishia matakwa yao; huku wakisahau kwamba amani ya Watanzania ni lulu wailindayo kwa udi na uvumba. Kwayo, shime ya mwalimu ilikuwa

ni kuwazindua Watanzania wasikubali kughilibiwa kwa vizawadi vitakavyowapelekea kuuza haki zao kama wapiga kura; lakini kuuza utu, heshima, amani na uhuru wa nchi yao.

**Ethosi (Sifa za Mneni)**

Hakika mwalimu alikuwa ni mtetezi wa wanyonge na mpiga vita rushwa (kitendo cha kuwatahadharisha Watanzania wajiepushe na vizawadi vya wanaotaka kuwanunua kijanja ili wawapigie kura; ambapo ni njia ya kuuza haki yao kifedhuli na kwa hivyo kujakupata bora viongozi na sio viongozi bora; kumaanisha wajiongeze kwa tafakuri pindi wanaposhauriwa hasa kuhusu mambo na uchaguzi wa viongozi wa nchi yao).

---

**Logosi (Maswali ya Kibalagha)**

*"... "Tunataka Rais wetu". Kwa Tanzania, haiwezekani ukampata Rais ambaye hana kabila.* ***Utampata wapi?****. Hatuwezi kuwa na Rais ambaye hana kabila. Atakuwa na kabila. Hatuta mkataa mtu kwa sababu ya ukabila wake.* ***Kumbe tutafanyaje?*** *Lakini, hatutamchagua mtu kwa sababu ya ukabila wake. Hatuwezi kumkataa mtu kwa sababu tunasema 'fulani tunaona anazo sifa za kuweza kuwa kiongozi wetu lakini ah! bwana ni Mkara! Mkara huyu sifa zote anazo lakini tunasema 'ah! Jamaa ni Mkara', hatutafanya hivyo. Hatutamkataa kwa sababu ya kabila lake. Tukifanya hivyo, tunafanya dhambi kubwa.* (uk 24:4/25:1: N).

**Pathosi (Hisia za Hadhira)**

Matumizi ya lugha yaliyomo katika (uk 24:4/25:1: N) ni balagha takriri yenye makataa ya Mwalimu kwa watanzania kwamba wasikubali kushawishiwa kupiga kura kwa vigezo vya udini na ukabila. Makataa ambayo yalihitaji ufafanuzi wa kidhana kwa Watanzania kujiulize "***… utampata wapi?*** (Kiongozi asiyekuwa na kabila au dini); na kwa papohapo mwalimu akizitagusa fikra zake tena akijibu kuuliza: ***"… kumbe tutafanyaje?*** – kwa jumla ya jawabu kwamba uzingatifu lazima uwe ni kwa kutathmini sifa za kiongozi bora mithali ya uzalendo wake, uadilifu na mwenye heba ya utetezi wa haki za wanyonge kwa muda wake wote wa maongozi yake. Kumaanisha kwamba uongozi kwake auone ni dhima ya kuwatumikia wale wote waliopo katika himaya yake bila kujali dini au makabila yao; huku akitambua kwamba kinyume chake atasababisha kutoweka kwa amani, upendo na ushirikiano katika jamii

**Ethosi (sifa za Mneni)**

Hakika kauli alizozitumia mwalimu zinadhihirisha uzalendo aliokuwa nao kwa nchi yake ya Tanzania. Alipenda umoja na amani kwa watu wote huku akichukulia udini na ukabila kama vyanzo vya utabaka na migawanyiko ya chuki katika jamii. Shime mwalimu Nyerere kupitia maongozi yake aliweza kuturithisha Watanzania misingi ya kudumisha amani, upendo na mshikamano baina yao

---

**Logosi (Maswali ya Kibalagha)**

*"(kutakiwa tukubali kwamba nchi yetu si ya wakulima wala wafanyakazi – nisahihi / ndiyo uhalisia)* ***... lakini sisi ni madodoki.?"*** (uk 22-23:1-2, HT3)

**Pathos (Hisia za Hadhira)**

Kauli ya mwalimu kuwaeleza Watanzania kwamba "***... lakini sisi ni madodoki.?*** Ni utumizi wa lugha ya picha ka Watanzania – kutathmini muktadha wa Azimio la Arusha ikiwa limepitwa na wakati kama wasemavyo miongoni mwao; huku neno "sisi" katika kauli hiyo ikidhihirisha nafsi ya kwamnza wingi; kumaanisha ukuruba wa mwalimu na Watanzania wenzake wanavyokongwa moyoni kwa yasemwayo kuhusu Azimio la Arusha ya kwamba leo yake haliwafai tena Watanzania. Mwalimu akiwawaona washawishi hao ya kwamba ni vibaraka wanaokiusha ukweli wa uhalisia wa mazingira ya Watanzania kwa manufaa yao binafsi. Na ndiposa mwalimu akiwauliza Watanzania wenzake ikiwa kukata misingi ya Azimio la Arusha ni sawa au ni sawa kwao kuwa sawa na madodoki.

Kwayo balagha aliyoitumia mwalimu ilikuwa ni kuwazindua Watanzania wahawilishe yale wanayoshawishiwa na vibaraka wanaolihujumu Azimio la Arusha ikiwa wayasemayo ni sawa na uhalisia wa mazingira yao; ikiwa nikweli leo yao nchi yao si ya wakulima na wafanyakazi tena na kwa hivyo suala la kuchapa kazi kwa juhudi na maarifa si muhimu tena – kwa maana ya misingi ya ujamaa na kujitegemea haina maana tena. Keifa amnbayo si kweli kwamba Tanzania si nchi ya wakulima na wafanyakazi; kumaanisha Azimio la Arusha hadi waleo yake lingali ni faafu na misingi yake ingali inahalisika na mazingira ya Watanzania. Kwayo kukatazwa azimio la Arusha ni kufanywa watu wabweteke wasifanye kazi kwa juhudi na maarifa, kwa kushirikiana ilhali nchi yao si tu kwamba ni ya wakulima na wafanyakazi lakini yenye neema ya: ardhi yenye rutuba, nguvukazi (wakiwemo Watanzania wanaoshawishiwa alibeue Azimio la Arusha) na uongozi bora ambao ndio mwalimu akiwatetea Watanzania – wasikubali kuumiwa na vibaraka wanaotaka kulihujumu taifa lao kwa utu na amali zilizomo.

**Ethos (Sifa za Mneni)**

Kauli hizi za Mwalimu zinadhihirisha uzalendo wake kwa taifa lake; lakini ukweli uaminifu kwa Watanzania wenzake (ambapo ndicho kiini cha kusema: "… lakini ***sisi sio madodoki*** (kwa maana ya Watanzania wasikubali kupokea kila waambiwalo bila ya kulitathmini)

---

**Logosi (Maswali ya Kibalagha)**

"*... Nchi zinaongozwa na watu, kumbe zinaongozwa na nani? Hakuna malaika. Ndivyo alivyotaka Mungu. Tujiongoze wenyewe: sisi hawa hawa. Lakini haziongozwi na akili za mtu. Zinaongozwa kutokana na sheria.*" (uk 14:2 N)

**Pathos (Hisia za Hadhira)**

Matamko hayo yamebeba maana nzito iliyokusudiwa kuwazindua Watanzania watambue wajibu wao kama wanadamu hapa duniani. Kwamba mbali na ushirikiano katika kuyatenda mambo ya kuwafaa katika maisha yao hawanabudi kuwa na kiongozi baina yao. Na ndiyo maana ya Mwalimu kusema: **" *... Nchi zinaongozwa na watu, kumbe zinaongozwa na nani?*** Kumaanisha kwamba, Watanzania ni watambue kwamba hakuna mtu au kiumbe chochote hata mfano wa "***Malaika***" atakayekuja kuwaongozea nchi yao, na kwa msisitizo akisema **"*hakuna malaika*"** kwa maana watambue kwamba, si katika utaratibu wa Mwenyezi Mungu kuwaagiza malaika duniani kwa ajili ya kuwatendea wanadamu majukumu yao, bali watambue ni wanadamu wenyewe, akisema: **"*ni sisi hawa hawa"*** kwa maana ya Watanzania wenyewe wajifunge kibwebwe wazitumie neema walizojaliwa na Mungu wao kama vile akili, afya, ukamilifu wa viungo na mazingira faafu washirikiane kwa pamoja katika kuyatenda majukumu yao ambapo kwa ufanisi wake ni waione ni dhima kumpata kiongozi wa kuwatangulia katika maamuzi na utendaji wa mambo yao kijamii.

Fauka ya hayo Mwalimu aliwatomelea Watanzania watambue kwamba mwanadamu si kitu fahari mbele ya Mwenyezi Mungu bali ni dhaifu na mwenye elimu kidogo tu aliyotunukiwa na Mwenyezi Mungu. Kumaanisha kwamba hawezi kuyaongoza mambo bila ya kuzingatia sheria. Ndiposa akasema: … ***(Nchi) Lakini haziongozwi na akili za mtu. Zinaongozwa kutokana na sheria.".*** kwayo, Watanzania walishawishiwa watambue kwamba wana dhima ya kuhakikisha kila unapowadia uchaguzi wa viongozi – wahusike kikamilifu katika kumpata kiongozi mwema na mwenye kufuata sheria zilizowekwa kwa minajili ya kudumisha umoja, upendo na amani miongoni mwao.

**Ethos (Sifa za Mneni)**

Hakika Mwalimu alikuwa ni hodari na mwenye mapenzi kwa nchi yake; ithibati ambayo tunaipata pale anaposema: (nchi haziongozi na malaika bali ni watu : ***ni sisi hawahawa***) *Lakini pia akiwataka watambue kwamba - haziongozwi na akili za mtu* bali *Zinaongozwa kutokana na sharia;* lakini aliyekuwa na mapenzi kwa raia (kwa alivyokuwa akiwataka washiriki kikamilifu katika kuwachagua viongozi wao ili wasijekujuta pale watakapo hisi kiongozi wao anaongoza kinyume na matarajio yao kumaanisha kwamba kujuta

hakutotokea ikiwa watamakinika kuwachagua viongozi bora na sio bora viongozi – kila unapowadia uchaguzi**.** Hakika hotuba hii ingali inawakumbusha Watanzania umakini aliokuwa nao mwalimu kuhusu maongozi ya nchi. Kwayo, kila uchao amekuwa ni kioo kwa Watanzania kumakinika kwa kila uchaguzi unapowadia minaajili ya kuwapata viongozi bora na sio bora viongozi. Shime mwalimu Nyerere kwa kuwazinduwa Watanzania kuhusu maongozi ya nchi.

---

**Logosi (Maswali ya Kibalagha)**

"*Rais tunayemtaka ni Mtanzania. Huwezi kumpata Rais Mtanzania asitoke ama Zanzibar ama Tanganyika. Anatoka ama Zanzibar ama Tanganyika, lakini hatumchagui kwa sababu ya Uzanzibari wake, hatumchagui kwa sababu ya Utanganyika wake. Na, akiuweka mbele Uzanzibari wake, akiuweka mbele Utanganyika wake, tunajua huyu mtu hatufai. …"* (uk 12:3/3:1: N). (anayegombea) *akichaguliwa, anaapishwa. Kama ni Mkristu, kwa Bibilia, kama ni Mwislamu, kwa Kuruani. Hatujachagua mtu asiyeamini Mungu, lakini tukimchagua, tutatafuta utaratibu wa kumuapisha. Ataapa! Hata asiyekuwa muumini, tutamwapisha kwamba atailinda na kuitetea Katiba ya Tanzania. Asipoilinda, tunajua ni msaliti. Tutamwapisha. Ataapa! lazima kabisa, hata kama si muumini. Kwa mujibu wa katiba yetu sisi, si lazima mtu awe anamwamini Mungu kuwa Rais, hata kidogo. Lakini, tutakuapisha! Umechaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu. Unaapa kulinda. Ataapa kwa huyo Mungu wake au akili yake anayoijua; lakini atatuapia. Ataapa kusudi tuweze kumshitaki kama akikiuka.*" (uk 13:3 / 14:1: N).

**Pathosi (Hisia za Hadhira)**

Nia ya Mwalimu kwa kauli hizi ilikuwa ni kuwataka Watanzania waitekeleze na kuisimamia katiba ya nchi yao pasi na kumhofia yeyote kwa wadhifa wake, kwa umaarufu wake au kwa eneo analotokea. Chembelecho uongozi kwa Watanzania; Mwalimu alisema: ***Huwezi kumpata Rais Mtanzania asitoke ama Zanzibar ama Tanganyika***. Kwa ufahima kwamba maadam Tanzania ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, yeyote mwenye sifa ya kuwa kiongozi wa Watanzania anaweza kutokea sehemu yoyote kati ya hizo mbili. Almuhimu ikiwa ana sifa za uongozi bora; ambapo kwa takriri neno alisema: "(Kiongozi wa Watanzania) ... ***hatumchagui kwa sababu ya Uzanzibari wake, hatumchagui kwa sababu ya Utanganyika wake. Na, akiuweka mbele Uzanzibari wake, akiuweka mbele Utanganyika wake, tunajua huyu mtu hatufai.*** Nia yake ni kukemea swala zima la ubaguzi hususani wa kieneo huku akiwatahadharisha Watanzania wote kuhakikisha kwamba wanailinda na kuiheshimu katiba ya nchi kikamilifu, wawachague viongozi kwa mujubu wa katiba; na viongozi waitumie katika maongozi ya nchi kama inavyoelekeza na siyo vinginevyo. Na ikiwa kiongozi atakwenda kinyume na inavyoelekeza katiba ya nchi; kwa maoni ya Mwalimu mtu wa namna hii ***hafai*** kuchaguliwa katika wadhifa wowote wa kiutawala.

Fauka ya hayo alitomelea kwa takriri balagha akisema: "***ataapa! … ataapa! Ataapa kusudi tuweze kumshitaki kama akikiuka.*"** Ufahima wa neno ***"kuapa"*** ni kiapo kwa mtu kuiweka roho yake rehani **-** kwa kujishitaki kwa Mwenyezi Mungu kwamba ikiwa atatenda kinyume na ukweli ulivyotakikana; Mwenyezi Mungu amlaani kwa kiapo chake; ampe adhabu ima kwa alivyojielekeza au kwa atakavyoamua mwenyewe Mwenyezi Mungu. Kiapo hicho ni mtawalio wa nafsi katika kuonyesha uzito wa jukumu la uongozi, kwamba, ni sharti ashike hatamu ya kuiongoza nchi kwa kufuata sheria zilizowekwa na sio kwa matashi binafsi. Hivyo, takriri neno "***kuapa***" pia ni changamoto kwa mtu na maamuzi yake ima kwa maswala yanayohusu uongozi kwa muktadha wa hotuba ya Mwalimu; kwamba sijambo rahisi bali ni zito na lenye hukumu ima kutoka kwa wanadamu wenyewe kwa wenyewe au kutoka kwa Mwenyezi Mungu peke yake. Na hii ndiyo kusema; Mwalimu alikuwa akiwashawishi Watazania watambue kwamba uongozi ni dhima inayohitaji umakinifu mkubwa na sio kwa mtu kuuonea gere kiasi cha hata kutoa hongo ili apate kuingia madarakani.

**Ethosi (Sifa za Mneni)**

Kauli aliyoitumia Mwalimu inabainisha ujasiri na uzalendo wa mwalimu kwa nchi yake ya Tanzania. Mwalimu alikuwa ni kiongoz ambaye katika maongozi ya yake alikemea utabaka (alipenda watu kuwa

wamoja) ndiposa akimaanisha kusema: "*Rais tunayemtaka ni Mtanzania. Huwezi kumpata Rais Mtanzania asitoke ama Zanzibar ama Tanganyika. Anatoka ama Zanzibar ama Tanganyika, lakini hatumchagui kwa sababu ya Uzanzibari wake, hatumchagui kwa sababu ya Utanganyika wake. Na, akiuweka mbele Uzanzibari wake, akiuweka mbele Utanganyika wake, tunajua huyu mtu hatufai. …"* (uk 12:3/3:1: N); lakini pia alikuwa imara katika kuchunga mbeko za nchi - katiba na sharia zake; kama alivyosema: "… *Kwa mujibu wa katiba yetu sisi, si lazima mtu awe anamwamini Mungu kuwa Rais, hata kidogo. Lakini, tutakuapisha! Umechaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu. Unaapa kulinda. Ataapa kwa huyo Mungu wake au akili yake anayoijua; lakini atatuapia. Ataapa kusudi tuweze kumshitaki kama akikiuka.*" (uk 13:3 / 14:1: N). kumaanisha alihakikisha raia na viongozi wa Tanzania hawavunji katiba ama sharia za nchi minaajili ya kulinda amani, upendo na utulivu wa nchi ya Tanzania. Hakika mwalimu Nyerere atakumbukwa na wengi milele na milele

---

**Logosi (Maswali ya Kibalagha)**

*" lakini kazi ya kujenga nchi hii kwa manufaa ya Watanzania wote ni kazi ya Watanzania, si kazi ya mtu mwingine. Msimamo huo tukauita Sisaa ya Kujitegemea. Msingi huo umekufa.* ***Hivi mmeshapata Mjomba?*** *Hivi kweli mtawadanganya Wafanyakazi kuwa msiwaambie 'chapeni kazi kama mnataka maslahi yenu yaboreshwe, tuchape kazi kwa faida yetu!' Tuache kuwaambia Wakulima kwamba 'kama tunataka maendeleo, tuchape kazi hivyo hivyo'. Hivi mtawaambia hawa kwamba 'tumeshapata Mjomba msiwe na wasiwasi!'* ***Mjomba huyo ni nani?*** *(uk 10:2, HT3)*

**Pathosi (Hisia za Hadhira)**

Huu ulikuwa ni ushawishi wa mwalimu kwa Watanzania akiwataka wazizindue fikra zao zisitekwe nyara na wale wasiolitakia mema taifa lao. Kutokana na utashi wa watu wchache waliokuwa wakiwashawishi Watanzania walikatae Azimio la Arusha ya kwamba limepitwa na wakati katika uhalisia wa Maisha yao. Ndiposa Mwamu kwa uzalendo wake akiwaonya kwa kuwataka watanabahi ikiwa wanavyoshawishiwa ni kweli; ndiposa akiwauliza: *"... lakini kazi ya kujenga nchi hii kwa manufaa ya Watanzania wote ni kazi ya Watanzania, si kazi ya mtu mwingine. Msimamo huo tukauita Sisaa ya Kujitegemea. Msingi huo umekufa.* ***Hivi mmeshapata Mjomba?*** *Hivi kweli mtawadanganya Wafanyakazi kuwa msiwaambie 'chapeni kazi kama mnataka maslahi yenu yaboreshwe, tuchape kazi kwa faida yetu!' Tuache kuwaambia Wakulima kwamba 'kama tunataka maendeleo, tuchape kazi hivyo hivyo'. Hivi mtawaambia hawa kwamba 'tumesha Mjomba msiwe na wasiwasi!'* ***Mjomba huyo ni nani?*** *…" (uk 10:2, HT3)* **-** wito, wa mwalimu kwa Watanzania ni wasikubali kushikiwa akili; wasikubali kuburuzwa kwa maslahi ya watu binafsi. Watanzania ni watambue kwamba hakutapatikana mtu wa kuwajengea ama kuwaletea maendeleo yao na ya taifa lao; zaidi watadanganyika na matokeo yake wabakie kujuta kwa majuto ambayo hayatawafaa tena kwa leo yao. Kwayo aliwashawishi watanznia wasikubali kulikana Azimio la Arusha kwani kulikataa ni kuuikataa misingiyake ya ujamaa na kujitegemea amabayo ni ndiyo mihimili ya ufaafu wa uhalisia wa maisha yakila siku yaliyowazunguka. Kwa hisia za moyoni mwao, Watanzania wakitashtiti kusema: hakika Mwalimu alikuwa mzalendo na mtetezi wa Watanzania kwa nguvu wote; lakini aliyejitoa muhanga kwa maneno na vitendo katika kuwaelekeza na kuwaongoza Watanzania kivitendo.

**Ethosi (Sifa za Mneni)**

Hakika Mwalimu alikuwa mkweli na mzalendo katika maongozi ya nchi; hakumchelea yeyote kwa lolote madam linakwenda kinyume na sera za nchi mintaarafu aliposema: ***Hivi mmeshapata Mjomba?*** *Hivi kweli mtawadanganya Wafanyakazi kuwa msiwaambie 'chapeni kazi kama mnataka maslahi yenu yaboreshwe, tuchape kazi kwa faida yetu!' Tuache kuwaambia Wakulima kwamba 'kama tunataka maendeleo, tuchape kazi hivyo hivyo'. Hivi mtawaambia hawa kwamba 'tumeshapata Mjomba msiwe na wasiwasi!'* ***Mjomba huyo ni nani?*** *(uk 10:2, HT3)* Alikuwa ni shujaa asiye tetereka na aliyekuwa na uoni wa mbali kuhusu Maisha na maendeleo ya jamii; kwayo, suala la kujitegemea Mwalimu alilihimiza kwa Watanzania huku akiwashawishi kutokana na uhalisia wa mazingira / maisha yao ya kila siku – aliwataka Watanzania

wachape kazi kwani kwa kufanya hivyo wataweza kuyahimu mahitaji yao na kuliletea maendeleo taifa lao; hakika Mwalimu alikuwa mzalendo na mtetezi wa wanyonge; lakini aliyejitoa muhanga kwa maneno na vitendo katika kuwaelekeza na kuwaongoza Watanzania kivitendo.

---

**Miishio ya Hotuba za Mwalimu Nyerere**

Ubainifu wa Makala haya ni kwamba, Mwalimu alikuwa akitakriri anuani ya hoja alizokuwa akiziibua na kuziendeleza. Kwa mujibu wa Assakakiy – kauli alizozitumia zote ni za balagha. Matumizi ya lugha aliyotumia yametoa picha halisi ya uweledi wake si tu kwa umahiri wake wa lugha lakini kudhihirisha kwamba alikuwa mwalimu kifani na ambaye daima alipenda kukazia marifa aliyoyaendelezaau la! Kwa mfano: alikuwa akizungumzia maswala ya muungano, akichimuza balagha takriri akisema: Muungano, uk. 12 ***…nimesema tuna ufa wa Muungano***. ***Ufa wa kwanza kabisa***. Katika ufa wa pili wa kutojali Katiba Uk. 14 anasema: "***Tumeona ufa huo wa kutojali Katiba ya nchi***" Katika ufa wa tatu wa kuendesha mambo bila kujali sheria uk. 15 anasema: "***…hatuwezi kuendesha mambo bila kujali Sheria***" Katika ufa wa nne wa Rushwa uk. 22 anasema: "***Sasa tunamtaka Rais anayekerwa na hilo…(rushwa).***" Katika ufa wa tano wa ukabila na udini uk. 30 anasema: "***… sasa yapo hayo … mambo ni mengi lakini kwa sasa ni hayo!***" Wakati ambapo Katika hotuba ya "***Tunatoka wapi, …***" amemalizia kwa taswira ya kuwakumbusha aliyoyazungumza na kwa mifano kama ishara ya ukolezo wa hotuba yake. Anasema: "***Sasa mfano mmoja nautumia mwisho kabisa...***" .

Kwayo, miishio yake daima ilikuwa ni ya kumfanya msikilizaji au msomaji kutafakari zaidi kutokana na takriri iliyokuwa ikijiri kila alipokuwa akifikia mwisho wa nukta ya msingi. Kwayo kupitia hotuza za mwalimu Nyerere, Makala haya yanabaini kwamba: mwalimu alikuwa ni mwenye kudumisha umoja, amani, upendo na mshikamano; alikuwa na kipaji cha hali ya juu katika ulingo wa uneni kisiasa; alikuwa mfasaha na mmakinifu katika kujenga hoja; lakini mwenye hoja zenye kuleta tafakuri kwa jamii; na kwamba hadi wa leo Watanzania wangali wakizitafakari na kuzifurahia hotuba zake kiasi cha kuzichukulia kama dira ya maongozi ya nchi yao. Na hii ndiyo kusema: ***Kilio cha Mwalimu*** kupitia hotuba zake ni ulumbi wa mambo mengi. Kwa mbiu ya **Sahau ukabila udini** aliweza kuwashawishi Watanzania kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao yote. Athari yake Watanzania wakashawishika, wakadumisha umoja, wakamng'oa Mkoloni, wakazalisha Jamuhuri yaMuungano wa Tanzania, wakapambana na maadui wa ndani (maradhi, ujinga na umasikini) na nje (vita dhidi ya Iddi Amini wa Uganda, msaada katika ukombozi wa nchi za Msumbiji, Angola, Afrika ya kusini na kadhalika). Umoja, amani na upendo vikawa ni vigezo mubashara kwa Watanzania kurejelewa na Walimwengu hadi wa leo. Shime! Waandishi, Wasomaji na Wasikilizaji wa hotuba za Mwalimu Nyerere.

## Marejeleo

Brown G., & Yule G. (1993) *Discourse analysis. Cambridge.* University Press.

Bizzell, P., & Bruce. H. (2000). *The Rhetorical tradition: Readings from Classical Times to the Present.* NY: Bedford.

Bloommaert, J. (1990) *Mordern African political style: Strategies and genre in Swahili political discourse.* In: *Discourse in Society*. London: SAGE.

Fogg, B. J. (2007). *Mobile persuasion: 20 Perspectives on the future of behaviour change.* Stanford. California: Standard Coprology Media.

Fogg, B. J. (2002). *Persuasive technology: Using computers to change what we think and we do.* Morgan Kaufman.

Garver, E. (1995) *Aristotle's Rhetoric: An Art of character.* The University of Chicago Press.

Kennedy & George (1991) *Aristotle on rhetoric: A theory of civic discourse.* Oxford: Oxford University Press.

Kiango, J. G. (2002) "*Nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa jamii mpya ya Afrika Mashariki*" *Nordic Journal of African Studies 11*(2): 185-197.

Leech, G. N. (1996). *A linguistic guide to English poetry*. London: Longman Group.

Masoud, M. N. (2010). *Uchanganuzi wa Taashira za kauli zilizoandikwa katika gari za Abiria Kisiwani Unguja*. M.A. Islamic University in Uganda.

Matasi B. (2014) *Uchanganuzi wa vitendo neni katika khutuba za Ijumaa na athari zake kwa waumini wa Bugisu*. M.A. Egerton University.

Mahochi, E. S. (2011) *"Mielekeo ya wasomi wa Kiswahili na viongozi wa Afrika Mashariki kuhusu lugha ya Kiswahili" Swahili Forum*, 18:2436.

Michael T. M. (2009) *Tutakukumbuka milele baba wa Taifa sisikazi. Economic Empowerment Centre*, Dar es Salaam.

Mizengo, P. P. (2009).*"Sherehe ya uzinduzi wa taasisi ya taaluma za Kiswahili"* Hotuba katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam". 27 Juni 2009.

Ogolla, A. R. (2007). *Uchanganuzi wa jinsi lugha inavyotumika kuhamasisha wanawake kuhusu haki zao: Mfano kutoka wilayani Kisumu.* Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Egerton.

Nyerere A. J., & Nkwera F. V. (2009). *Mtumishi wa Mungu – J. K. Nyerere, Namna bora ya kumwenzi*. Marian Faith Healing Centre, Dar es Salaam.

Taasisi ya Mwalimu J. K. Nyerere (1995). *Nyufa,* Dar es Salaam.

------------------------------------------ (1995). *Tumetoka wapi, Tuko wapi na Tunakwenda wapi. Dar* es Salaam.